**MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA**

**Karatasi ya Maswali: namba 13**

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa ‘Kazi ya ziada’, unaweza kulijibu swali kama unapenda, au kuliacha kama unaona ni gumu mno. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

**MASOMO: 49 - 52**

37.(a) Ni nani aliyekuwa mtume mkubwa zaidi?
   (b) Tunawezaji kutambua kama dhamira iliyopo ndani ya mtu ni kiburi au tamaa?
   (c) Kwa nini Yesu aliwaosha wanafunzi wake miguu yao?
   (d) Wale walio na majukumu mbalimbali kwenye Eklesia wanatambulika kuwa ni ‘watumishi’. Fafanua.

Kazi ya ziada
   (e) Tunaweza kujifunza nini kulingana na mfano wa Hamani?

38.(a) Ni kwa namna gani Anania na Safira walikiuka utaratibu?
   (b) Wajibu wa ‘nuru ya kweli’ ni nini?
   (c) Tulipe kodi?
   (d) Mzee wa Eklesia (kanisa) aweje?

Kazi ya ziada
   (e) Ni nini malipo ya uongo?

39.(a) Hasira ni mbaya?
   (b) Mungu anachukia?
   (c) Mungu anafikirije juu ya kuvunja ahadi na kudanganya kwa makusudi?
   (d) Kama ukisema maneno makali kwa hasira, unasuluhishaje?

Kazi ya ziada
   (e) Yesu aliwatimua wauzaji kwenye hekalu. Je, ilikuwa dhambi?

40. (a) Kama serikali yako ni mbovu, unapaswa kulipa kodi?
   (b) Tufanyeje kama tunaitwa kujiunga na jeshi?
   (c) Ni sawa kwa Mkristo kujihusisha na siasa?
   (d) Mkristo afanyeje kama akitakiwa awe ‘mzee’ wa mahakama?

Kazi za ziada
   (e) Kama ukitakiwa kupiga kura kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa CBM, utachaguaje?
   (f) Unafikiri ni sawa kwa wanajumuia wa CBM kupata kura kwa kupiga kampeni?

*Kumbuka kuweka jina lako, anwani na namba yako ya kumbukumbu katika karatasi yako ya majibu.*